



Na Rais
Susan H. Porter
Rais Mkuu wa Msingi

UHUSSIANO WA AGANO

Rais Nelson alifundisha kwamba Baba wa Mbinguni anao upendo maalumu kwa wale wanaofanya Naye maagano.* Tuna-pobatzwa na kuthibitishwa, tunaahidi kuwa watiifu na waaminifu Kwake. Yeye anafanya ahadi sawa na hiyo kwetu.

Baba wa Mbinguni na Yesu Kristo wanakupenda sana. Kwa saba-bu Wanakupenda, wamekualika ufanye Nao maagano au ahadi. Unanza kuwaka ahadi hizo wakati unapobatzwa.

Baada ya ubatzizo wako, unapokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Unakuwa muumini wa Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho. Hiyo humaanisha Baba wa Mbinguni anakuumini wewe kutii maagano yako.

Ni kipi unaweza kufanya kama muumini kamili wa Kanisa ili kutunza maagano yako? Unaweza kuwakaribisha wengine kwenye darasa la Msingi. Unaweza kuketi kando ya mgeni na kuwasaidia wajifunze nyimbo. Unaweza kusaidia kwenye shughuli za Msingi. Unaweza pia kuwa kiongozi katika familia yako. Unaweza kuomba muwe na sala ya familia au kushiriki kile ulichojifunza katika darasa la Msingi.

Baada ya kupokea Roho Mtakatifu, unaweza kuyaona mahitaji ya wengine katika namna mpya.

Unaweza kusali kwa Baba wa Mbinguni na kusema, "Nisaidie nijue nani ninaweza kumsaidia leo." Kisha Roho Mtakatifu anaweza kukusaidia umtambue mtu aliyeketi peke yake au kukuambia umjulie hali rafiki. Unalata tofauti kubwa wakati unapochagua kuwasaidia wengine. Unatenda kama muumini wa Kanisa la Baba wa Mbinguni!

Baba wa Mbinguni anakupenda. Anakutaka uongoze kwa mfano popote unapoenda ili uweze kuwaleta wengine karibu Naye. Lakini hupaswi kufanya hilo peke yako. Baba wa Mbinguni na Yesu Kristo kamwe hawataacha kukusaidia. Unaweza kuhisi ujasiri kwa sababu unajua Wapo pamoja nawe. Unaweza kumfikiria Yesu Kristo daima amesimama kando yako. ●

Kutoka kwenye mahojiano na Olivia Kitterman na Rachel Peterson.


**Je, nani ninaweza
kumsaidia leo?**

**Andika mawazo yako
kwenye mnyororo wa
karatasi!**



Mnyororo wa Marafiki

1. Kata na uondoe sehemu nyeupe upande wa kulia. Au chora mtu kwenye karatasi nyingine ili ukate.
2. Kunja kufuata mstari kwenda nyuma na mbele kama vile pangaboi.
3. Kata na uondoe mistari iliyokunjwa ya mipaka ya mtu.
4. Ifungue ili kuona mnyororo wa marafiki wakiwa wameshikana mikono! Wapambe waonekane kama watu unaowapenda.



VIELELEZO NA JARED BECKSTRAND



*"Agano la Milele," *Liahona*, Okt. 2022, 4-11.